# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



## JARIDA MAALUMU JUNI, 2021


BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Mwenyekiti

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAANDISHI**
Munir Shemweta
Eliafile Solla
Hassan Mabuye
Magreth Lyimo



Mji wa Serikali Mtumba, S. L. P. 2908 | 40477- DODOMA | Simu: +255 262 963309/13/14 | Nukushi: +255 262 963316
Barua pepe: ps@lands.go.tz | Tovuti: www.lands.go.tz




*Balozi wa Marekani nchini Tanzania Dk. Donald Wright akimkabidhi zawadi ya kitabu Waziri wa Ardhi Mhe. Lukuvi kinachoelezea jimbo la Texas ambako ndipo Balozi huyo anapotokea alipomtembelea ofisini kwake Mtumba - Dodoma*

# SERIKALI KURASIMISHA ASLIMIA 35 YA VIPANDE VYA ARDHI IFIKAPO 2025

**Na Lusajo Mwakabuku**

Serikali inatarajia kuongeza kasi ya Kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ambapo moja kati ya melengo yanayotarajiwa ni pamoja na kurasimisha asilimia 35 ya vipande vya ardhi nchini ifikapo mwaka 2025 ikilinganishwa na hali ya sasa ambapo ni asilimia 25 ya vipande vya ardhi nchini vimerasimishwa.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri mwenye dhamana nchini Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 16, Juni 2021 alipotembelewa na Balozi wa Marekani nchini Tanzania Dk. Donald Wright ambaye yupo katika ziara yake ya kutembelea wizara mbalimbali Mkoani Dodoma.



*Katibu Mkuu wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi (wa tatu kutoka kushoto) pamoja na wafanyakazi wa Ubalozi wa Marekani wakifuatilia mazungumzo kati ya balozi wa Marekani na Waziri wa Ardhi katika Ofisi za Ardhi zilizopo Mtumba Mkoani Dodoma*

Mhe. Lukuvi alimueleza Balozi kuwa Wizara inaendeleza hatua mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kubuni miradi mbalimbali kupitia fedha za ndani lakini pia kupitia wahisani ambao kwa pamoja wanaazimia kuhakikisha kila kipande cha ardhi nchini kimepimwa.

“Miradi inayoendelea hivi sasa ni pamoja na kuweleza nguvu katika kurasimisha makazi holela ambayo sehemu kubwa ya wananchi wanamiliki vipande vya ardhi visivyopimwa na hawana nyaraka za umiliki” Aliongeza Lukuvi.

Aidha Lukuvi akachukua nafasi hiyo kumueleza Balozi Wright kuwa jitihada hizi zinakwamishwa na ukuaji wa teknolojia ambapo watumishi wengi wamekutana na changamoto katika kuendana na teknolojia na hivyo akamuomba Balozi Wright kuangalia namna ya kuwawezesha watumishi kwa kuwapatia mafunzo kadri inavyowezekana.

“Sisi hatuna shida na kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kazi za upimaji ardhi, shida inakuja pale ambao kunakuwa mitambo ya kisasa lakini bado tunakosa watu wenye utaalamu wa kutoa wa kuitumia mitambo hiyo ipasavyo. Kama utasikia sehemu yoyote kuna chuo au mafunzo yawe ya muda mrefu au mfupi tupo tayari kushiriki ili tuwawezeshe watu wetu kiutaalam” Lukuvi




*Balozi wa Marekani nchini Tanzania Dk. Donald Wright akipiga picha na Waziri wa Ardhi Mhe. Lukuvi mbele ya ofisi za jengo la Wizara ya Ardhi Mtumba Dodoma*

Akijibu hoja hiyo ya Waziri, Balozi Wright alisema analichukua hilo swala na kulifanyia kazi na akawaagiza watu alioambatana nao kuangalia ni namna gani wanaweza kushirikiana kwa pamoja na wizara katika kuhakikisha kasi ya upimaji, upangaji na umilikishaji ardhi nchini inaongezeka na kuboreka.

Akielezea jinsi hali ilivyo Marekani, Balozi Wright alisema wao wako katika nafasi nzuri zaidi ya kutoa mwongozo kwani makazi yao yamepimwa na kupangwa kwa asilimia 100 na kwamba eneo lolote haliwezi kuuzwa bila ya kuwa na nyaraka sahihi (hati) za umiliki.

# ITILIMA WAPEWA ELIMU YA UMILIKI ARDHI

**Na Mwandishi Wetu, SIMIYU**

Wakazi wa kijiji cha Itwimila B kilichopo kata ya Kiloleli Wilayani Busega mkoani Simiyu wamepata elimu ya haki ya umiliki ardhi kwa wataalam wa ardhi kutoka Ofisi ya Mkoa na Wilaya.

Elimu hiyo ilitolewa tarehe 02 Juni 2021 kwenye mkutano uliofanyika kijiji cha Itilima B mkoani Simiyu chini ya uongozi wa kijiji hicho na msisitizo mkubwa wakati wa utoaji elimu hiyo ulikuwa ni haki ya umiliki wa ardhi.

Bw. Jephta Msuta, Afisa Ardhi mkoa wa Simiyu akizungumza wakati wa kutoa elimu hiyo, alisema umiliki wa ardhi unaotambulika kisheria ni ule unaothibitishwa kwa mwenye ardhi kuwa na hati miliki.

Kwa mujibu wa Bw. Msuta, hati miliki ni kitambulisho cha kisheria kinachothibitisha uhalali wa umiliki wa ardhi, huku akitaja baadhi ya faida za hati miliki kuwa ni kuepuka migogoro ya ardhi na kupata fursa ya mikopo kutoka kwa taasisi za kifedha.

Kwa upande wake Afisa Mipango Miji mkoa wa Simiyu Bw. Steven Mkude alisema, suala ya upangaji miji katika eneo lolote ni jambo la msingi katika kutambua makazi na kuweka wazi kuwa, pale panapokuwa na uhitaji wa mtu kupimiwa ardhi basi ni jukumu la afisa anayehusika kufanya hivyo.



*Afisa Ardhi wilaya ya Busega Bw. Martin Bantazuka akitoa elimu juu ya masuala ya umiliki wa ardhi katika kijiji cha Itwimila B, wilayani Busega, Simiyu.*

Naye Afisa ardhi wa Wilaya ya Busega Bw. Martin Bantazuka aliwatoa hofu wananchi wa kijiji hicho waliolipa fedha wakati wa zoezi la upimaji kwa kuwaeleza kuwa, kumbukumbu za nyaraka kuhusiana na zoezi hilo zipo hivyo hawapaswi kulipa tena fedha.

Aidha, Bw. Bantazuka alibainisha kuwa, wakati wa kupitia maeneo yote yaliyopimwa wataangalia miundombinu iliyowekwa sambamba na alama za upimaji ili kujiridhisha na kufanyia marekebisho.

Wakazi wa kijiji hicho Itwilima B walitoa shukrani zao kwa wataalam wa ardhi ngazi ya mkoa na Wilaya kwa kuwatembelea na kufanya nao kikao na kuomba matatizo ya ardhi yashughulikiwe kwa uharaka.

Hata hivyo, wakazi wa kijiji hicho wamekiri kuwa, migogoro mingi ya ardhi inatokana na kutokuwa na elimu hasa ya umiliki wa ardhi kwa wakazi wengi na kuomba wataam wa ardhi waendelee kutoa elimu kwa wananchi ili kumaliza migogoro ya ardhi.



*Afisa Ardhi Mkoa wa Simiyu Bw. Jephta Msuta akitoa elimu juu ya masuala ya umiliki wa ardhi katika kijiji cha Itwimila B, wilayani Busega, Simiyu.*



*Afisa Mipango Miji Mkoa wa Simiyu Bw. Steven Mkude akitoa elimu juu ya utaratibu wa mipango miji katika kijiji cha Itwimila B, wilayani Busega, Simiyu.*



*Afisa Ardhi wilaya ya Busega Bw. Martin Bantazuka akitoa elimu juu ya masuala ya umiliki wa ardhi katika kijiji cha Itwimila B, wilayani Busega, Simiyu.*



*Sehemu ya wakazi wa kijiji cha Itwimila B wakisikiliza kwa umakini maelezo kutoka kwa wataam wa ardhi kuhusu umiliki wa ardhi katika kikao kilichofanyika katika kijiji hicho.*



*Wananchi wa Kata ya Matumbulu mtaa wa Kusena mkoani Dodoma wakisikiliza kwa makini maelekezo kutoka kwa wataalamu juu ya zoezi zima la upangaji na upimaji linalotarajiwa kuanza hivi karibuni.*

# NEEMA YANUKIA KATA YA MATUMBULU - DODOMA



*Afisa Mipango Miji Mwandamizi Bw. Mtaki Fab akiwaelimisha zaidi wananchi wa mtaa wa Kuse kuhusu zoezi la upangaji na upimaji*

## Na Magreth Lyimo

Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Dodoma imeendelea kutoa elimu kwa wananchi wa Kata ya Matumbulu yenye mitaa saba juu ya zoezi la kupanga, kupimwa, kumilikishwa mpaka hatua ya mwisho ya kupatiwa hati.

Wananchi wa Mtaa wa Kusena Kata ya Matumbulu walipata neema hiyo mwanzoni mwa wiki hii ambapo maafisa kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na maafisa kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma walipotembelea mtaa huo na kutoa elimu ya kupanga na kupima pamoja na kuelezea faida zake iliyopelekea wananchi kukubaliana na zoezi la urasimishaji na upimaji shirikishi ambalo litaanza pindi mitaa yote ya Kata ya Matumbulu kupata elimu juu ya upangaji na upimaji.

Afisa Mipango Miji Mwandamizi Bw. Mtaki Fabian alisema kuwa kulingana na master plan ya jiji la Dodoma iliyopitishwa mwaka 2019 maeneo ya kata ya matumbulu ni maeneoyaliyotengwa kwa ajili ya mashamba. Lakini kabla ya master plan kuna maisha ambayo tayari watu walikuwa wanaishi hivyo ikaamuliwa kwamba yale maeneo yatapangwa na kurasimishwa kama maeneo ya makazi.

Hata hivyo Bw. Fabian alieleza kuwa zoezi hilo likikamilika mwananchi ataweza kupata mikopo benki na pia atakuwa na uwezo wa kuendeleza eneo lake. Lakini pia eneo likishapimwa ni rahisi kujua barabara pamoja na shughuli za kijamii zinapita wapi hivyo kuleta maendeleo katika sehemu husika.

Katika hatua zote za upangaji na upimaji Afisa Mipango Miji kutoka Ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma Bw. William Alphayo alisema kuwa zoezi hilo litazingatia mahitaji halisi yaliyoainishwa na wataalamu kwa kushirikiana na kamati ya upimaji shirikishi ambayo wananchi wa mtaa husika huchagua wawakilishi watakaounda kamati hiyo.

Bw. Kedimoni Lenadi Masenha ambae ni mkazi katika mtaa wa Kusena alisema kuwa hatua hii ya urasimishaji ikianza na kumalizika vizuri basi itasaidia sana katika kupunguza migogoro ya ardhi pamoja na kuchochea maendeleo katika Kata ya Matumbulu .

Wakina mama nao hakuwa mbali katika utekelezaji wa mradi huu ambapo Bi. Mariam Mpali ambae pia ni mjumbekatika Kamati ya Upimaji Shirikishi Mtaa wa Kusena alisema kuwa mradi huo ni mzuri na utawasaidia watoto kusoma kwa sababu akipata hati ataweza kukopa na kuendeleza watoto wake kielimu.



*Afisa Mipango Miji kutoka Ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma Bw. William Alphayo akitoa elimu kwa wananchi wa mtaa wa Kusena*

# DODOMA KUANZA KUTOA HATIMILIKI ZA ARDHI ZA KIELEKTRONIK JULAI MOSI 2021

Na Munir Shemweta, WANMM DODOMA



*Mbunge wa Jimbo la Dodoma Anthony Mavunde akimkabidhi hati ya pamoja Bi. Zawia A. Ally katika zoezi la utoaji hati miliki za ardhi kwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao katika mitaa ya Miganga na Chinyika Kata ya Mkonze Jijini Dodoma*

Ofisi ya Ardhi mkoa wa Dodoma itaanza kutoa hatimiliki za ardhi za Kielektroniki kwa wamiliki wa ardhi  kuanzia Julai mosi, 2021.

Hayo yamebainishwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Dodoma Thadei Kabonge wakati wa utoaji hati za ardhi kwa wananchi waliorasimishiwa maeneo yao kwenye mitaa ya Miganga na Chinyika katika kata ya Mkonze mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki.

Kwa mujibu wa Kabonge, kwa sasa ramani zote za mkoa wa Dodoma zipo kwenye mfumo wa kijiditali hivyo ofisi yake itaanza kutoa hati za ardhi za kielektroniki kwa kuwa hati hizo ziko katika nakala laini.

Kwa sasa Hati za Kielektroniki nchini zinatolewa kwenye manispaa nne za mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni Ilala,Temeke, Kinondoni na Ubungo na hati hiyo ni ya kurasa moja.

"Ramani zote za dodoma kwa sasa zipo kidigitali na julai mosi mwaka huu tunaanza kutoa hati za kieleltroni maana hati zote ziko katika nakala laini" alisema Kabonga.

Aliwataka wakazi wa Dodoma wanaomiliki ardhi kuhakikisha wanapimiwa maeneo yao na kupata hati kwa kuwa gharama za upatikamaji hati sasa imepungua  ukilinganisha na miaka ya nyuma na kusisitiza kuwa lengo la ofisi yake ni wananchi wanaomiliki ardhi katika jiji la Dodoma kupata hati zao.

Katika kuhakikisha ardhi ya jiji la Dodoma inapangwa na kupimwa, Kamishna huyo wa Ardhi Msaidizi mkoa alisema, ofisi yake ilipeleka timu ya wataalamu katika mitaa mbalimbali ikiwemo ya Miganga na Chinyika kwa lengo la kupima maeneo lakini muitikio umekuwa mdogo kiasi cha kuamua timu hiyo kuondoka kwa baadhi ya maeneo.
Naye Mbunge wa jimbo la Dodoma Anthony Mavunde  aliyekuwa mgeni rasmi katika zoezi la kugawa hati kwa wananchi wa mitaa ya Miganga na Chinyika alilielezea tukio la utoaji hati kwa wananchi waliorasimishiwa maeneo yao kuwa ni tukio la kihistoria kwa kuwa hati zinawafuata wananchi katika maeneo yao badala ya wao kuzifuta
Alisema, hatua ya kupanga na kupima ardhi katika jiji la Dodoma unaofanywa na Wizara ya Ardhi  Nyumba na Maendeleo ya Makazi unalifanya jiji hilo kupimwa kwa kasi na kupunguza ongezeko la makazi holela, thamani ya ardhi kupanda sambamba na kuondoa migogoro ya ardhi.

"Leo ni furaha mji unapimwa kwa kasi unaondoa uholela, kuongezeka thamani ya ardhi pamoja na kuondoa migogoro, ukipima eneo unatatua changamoto zote na dododma ikipimika na kupangwa vizuri inakuwa sura ya makao makuu" alisema Mavunde.

Mavunde aliwaeleza wananchi wa mitaa ya Miganga na Chinyika kuwa hati waliyopewa inawapa uhakika wa miliki pamoja na hati hiyo kutumika na taasisis za kutoa mikopo kwa wananchi.
Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji wa halmashauri ya jiji la Dodoma William Alfayo alisema, kazi ya upangaji na upimaji iliyofanyika kwenye mitaa miwili ya Miganga na Chinyika mkoani Dodoma ni sehemu ya kazi inayofanyika kwenye kata zote za jiji la Dodoma na zoezi hilo linafanyika kwa mujinbu wa mpango kabambe wa jiji la Dodoma 2019 hadi 2039 .

"Tusisahau kilimo cha zabibu katika mipango yetu, sisi tunaendelea  na upangaji na upimaji wa mashamba ya zabibu katika maeneo ya Mjini na ninatoa wito kwa wana Dodoma kuzingatia uwekezaji katika zao la zabibu ikiwemo uchakataji wa zao hilo" alisema Alfayo



*Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma Thadei Kabonge akizungumza katika zoezi la utoaji hati miliki za ardhi kwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao katika mitaa ya Miganga na Chinyika Kata ya Mkonze Jijini Dodoma*



*Mbunge wa Jimbo la Dodoma Anthony Mavunde (aliyevaa kofia) akiwa katika picha ya pamoja na wananchi waliokabidhiwa hati katika zoezi la utoaji hati miliki za ardhi kwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao katika mitaa ya Miganga na Chinyika Kata ya Mkonze Jijini Dodoma*

# UPANGAJI MAENEO YA MRADI WA SGR WASHIKA KASI

**Na Munir Shemweta**

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na ofisi za ardhi katika mikoa inayopitiwa na mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) imeendelea na zoezi la kupanga na kupima maeneo inayopita reni hiyo kwa kasi ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza pamoja na kuanisha maeneo ya uwekezaji.

Zoezi hilo kwa sasa linaendelea kwenye maeneo ya vituo vya Pugu -Dar Es Salaam, Soga na Kwala mkoani Pwani, Ngerengere na Kilosa mkoani Morogoro, eneo la Ihumwa Dodoma pamoja na Makutopora Singida.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Makazi Sehemu ya Usanifu na Mapango wa Miji Wizara ya Ardhi Bi. Imacultae Senje, kazi inayofanywa ni kuyapanga maeneo yote yanayopitiwa na Reli ya Kisasa (SGR) husan maeneo ya vituo yaliyo na fursa kwa wananchi.

Akielezea kazi zinazofanyika kwenye mkoa wa Pwani hivi karibuni, Bi Senje alisema, katika mkoa huo timu yake inandaa michoro ya mipango miji mitatu yenye viwanja vya ukubwa mbalimbali 127 vya uwekezaji hasa viwanda na kubainisha kuwa kazi ya upimaji imeshakamilika ikiwemo mchoro mmoja wenye ukubwa wa ekari 2500



*Wataalam wa Mipangomiji kutoka Makao Makuu ya Wizara Dodoma wakibadilishana mawazo kuhusu rasimu ya mpangokina wa eneo la uwekezaji iliyoandaliwa kwa kushirikiana na wataalam wa Ofisi ya Kamishna Mkoa wa Pwani, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na Kituo cha Uwekezaji (TIC)*

Hata hivyo, alisema changamoto katika mkoa wa Pwani ilikuwa eneo la Kwala iliyohusisha migogoro ya mipaka kati ya eneo la serikali na vijiji vinavyozunguka eneo la uwekezaji chini ya Wizara ya Mifugo ambapo alisema usuluhishi wake unaendelea vizuri.

Akielezea kuhusu eneo la kituo cha Pugu mkoa wa Dar es Salaam, Mkurugenzi huyo Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi Wizara ya Ardhi sehemu ya Usanifu na Mapango Miji, alisema kazi inayofanyika katika eneo hilo ni kuanisha eneo la reli na kulipima ili lisivamiwe.
Pia alielezea kazi inayofanyika eneo ya Ihumwa Dodoma na Makutupora Singida na kufafanua kuwa kuwa, kwenye eneo la Ihumwa kazi kubwa inayofanyika ni urasimishaji makazi holela huku eneo la Makutupora Singida wakitambua maeneo yaliyopangwa na kupimwa.

Aidha, Bi. Senje alisema muitikio wa wananchi katika zoezi hilo kwa maeneo yote ni mzuri kwa kuwa unatoa fursa kwa wananchi wanaozunguka mradi huo wa kimkakati kwa lengo la kukuza shughuli zao za kiuchumi na kibiashara.

Ujenzi wa Reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutopora Singida unafanyika kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inaanzia Dare es salaam hadi Morogoro na kuhusisha vituo sita vya Dar es Salaam, Pugu, Soga, Ruvu, Ngerengere na Morogoro huku vituo vya Dar es Salaam na Morogoro vikiwa vituo vikubwa.



*Mpima Ardhi wa Mkoa wa Pwani, Bi Nina Rutakyamirwa (aliyeshika ramani na aliyevaa blouse ya brown), akiongoza timu ya Wapima Ardhi katika upimaji wa eneo la uwekezaji la Kwala lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.*



*Wataalam wakifanya majadiliano na viongozi mbalimbali wa Kijiji na Kata kabla ya kuanza kazi ya utambuzi wa mipaka*



*Wataalam wakiendelea na kazi ya utambuzi wa mipaka eneo la uwekezaji.*